JUMUIYA YA TAWALA ZA MITAA TANZANIA

(ALAT)

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC)

UZOEFU KUTOKA BARAZA LA BIASHARA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

Uzoefu Kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa

Uanzishaji wa Baraza la Biashara la Wilaya

Mkoa wa Dodoma-Tanzania

Ripoti ya Mradi Imeandaliwa
na

Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT)
S.L.P. 2049
DODOMA

Imefadhiliwa na

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC)

Kwa kushirikiana na

Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT)

Na

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa

Agosti, 2018

YALIYOMO

SHUKRANI ..... *i*

ORODHA YA VIFUPISHO ..... *ii*

SURA YA KWANZA *1*

UTANGULIZI *1*

1.1 Usuli *1*

SURA YA PILI *4*

UFUMBUZI WA TATIZO *4*

2.0 Utangulizi *4*

2.1.1 Malengo ya Mradi *4*

SURA YA TATU *6*

MAFANIKIO, CHANGAMOTO, VIKWAZO, UIMARA NA MAFUNZO KUTOKA KATIKA MRADI *6*

3.0 Matokeo na Mafanikio ya Mradi *6*

3.3. Mipango ya Uimarishaji wa Mradi *8*

3.4. Mafunzo Kutoka katika Mradi *9*

SURA YA NNE *10*

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO *10*

4.0 Hitimisho *10*

4.1 Mapendekezo *10*

SHUKRANI

Andiko hili linafahamika kama Mradi wa Ufufuaji wa Baraza la Biashara la Wilaya. Andiko hili ni muendelezo wa maandiko kuhusu miradi ya mfano ambayo ipo chini ya ALAT kwa ufadhili wa LIC.

Halmashauri ilifanya juhudi ya kufufua jukwaa la Baraza la Biashara ya Wilaya kwa minajili ya kutumia jukwaa hilo kuunganisha sekta binafsi na mamlaka za serikali kutatua kero mbalimbali za kibiashara.

Ninapenda kutumia nafasi hii kuushukuru Ubalozi wa Denmark kwa msaada wao wa fedha kupitia mradi wa LIC ambao umewezesha kupatikana fedha za kuandaa na kuchapisha andiko hili.

Tunatoa shukrani za kipekee kwa mratibu wa mradi wa LIC, Bw. Flemming Winther Olsen na timu yake kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na washikadau wa kitaifa kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu, OR-TAMISEMI, TNBC, TPSF na TCCIA.

Pia, tunatoa shukrani kwa uongozi wa mkoa wa Dodoma, uongozi wa Halmshauri ya wilaya ya Kongwa, wajumbe wa Baraza la Biashara la Wilaya kwa kutupatia taarifa zilizosaidia kukamilika kwa andiko hili.

Mwisho, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa ALAT na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI hasa Bi. Husna A. Kandoro, Vicent Chomola na Anicetus Mramba kwa ukusanyaji wa taarifa zilizosaidia kupatiakana kwa andiko hili.



Abdallah S. Ngodu

Kaimu Katibu Mkuu– ALAT

ORODHA YA VIFUPISHO

ALAT	Association of Local Authorities of Tanzania
DBCs	District Business Councils
DC	District Council
KDC	Kongwa District Council
LGA	Local Government Authorities
LIC	Local Investment Climate
OsBC	One Stop Business Centre
PPD	Public Private Dialogue
PO – RALG	President's Office Regional Administration and Local Government
TBS	Tanzania Bureaus of Standards
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture
TNBC	Tanzania National Business Council
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation
VETA	Vocational Educational and Training Authority

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli

Halmashauri ya Wilaya Kongwa ni moja kati ya Halmashauri saba (7) zinazounda mkoa wa Dodoma. Halmashauri zingine ni pamoja na Chamwino, Kondoa, Mpwapwa, Chemba na Jiji la Dodoma. Chamwino ipo katika latitudo 5° 30- 6° Kusini na longitudo 36° 15° – 36 Magharibi mwa Griniwichi. Kwa upande wa mwinuko, eneo hili lipo baina ya mita 900 na 100 kutoka usawa wa bahari. Mji wa Kongwa ndiyo makao makuu ya wilaya hii na upo umbali wa km 86 kutoka jiji la Dodoma.

Kwa upande wa mipaka, Halmashauri ya Kongwa inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa upande Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto (mkoa wa Manyara) kwa upande wa Kaskazini, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (mkoa wa Morogoro) kwa upande wa Magharibi na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa upande wa Kusini.

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina tarafa tatu ambazo ni Mlali, Kongwa na Zoissa. Pia, inazo kata 22, vijiji 74 na vitongoji 312. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina jumla ya wakazi 318,995, kati yao watu 156,982 ni wanaume na watu 162, 013 ni wanawake. Ongezeko la watu kwa mwaka ni wastani wa asilimia 2.4.

Kwa asili, mazao (ya chakula na biashara) yanayostawi katika eneo hili ni pamoja na mahindi, mtama, karanga, mihogo, alizeti, maharage, mbogamboga (hasa kandokando ya mito iliyopo katika vijiji vya Tubugwe na Chamkoroma).

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina maeneo ya miji/senta kama vile Kongwa, Mlali, Mkoka, Pandambilli, Mbande, Hembahemba na Kibaigwa. Mji wa Kibaigwa ni sehemu maarufu sana kwa sababu ya kuwepo kwa soko la kimataifa la mahindi kwa ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

1.2 Ufafanuzi Kuhusu Mradi

Mnamo Novemba 20 mwaka 2014 LIC ilianza rasmi miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa baada ya kukamilika kwa maandiko mradi wa LIC ulitoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali. Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa iliandaa maandiko ya miradi ipatayo 21 na kuyawasilisha kwa LIC kwa ajili ya kuyapitisha. Kati ya maandiko hayo, miradi 7 ilifanikiwa kupata fedha kutoka LIC.

Miradi iliyofanikiwa kupata fedha kutoka LIC ni pamojana Mradi wa Kituo Kimoja cha Biashara (*One Stop Business Centre* (OsBC), Mradi wa Soko la Mbogamboga Kibaigwa, Mradi wa Utunzaji wa Kumbukumbu/Kanzi Data, Mradi wa Ufugaji Kuku wa Kongwa na Mbande, Mradi wa Kituo cha Biashara ya Alizeti Pandambili, Mradi wa Ujenzi wa Soko la Biashara Mkoka, na Mradi wa Uboreshaji wa Mnada wa Mbande.

Ili kuhakikisha kuwa miradi ya LIC inafanikiwa, kulifanyika tathmini ya hali ya kibiashara katika Halmashauri kwa minajili ya kuona fursa na changamoto zilizopo ndani ya Wilaya. Hivyo basi, LIC kwa kushirikiana na wafanyabiashara waliamua kulifufua Baraza la Biashara la Wilaya (DBC) kwa lengo la kushughulikia changamoto zote za kibiashara zilizopo katika Halmashauri.

Mnamo mwaka 2014 LIC iliamua kufadhili uanzishwaji rasmi wa Baraza la Biashara la Wilaya ambalo lililenga kujadili na kutatua changamoto zote za kibiashara zilizopo katika Halmashauri husika. Baraza la Biashara la Wilaya ya Kongwa lina wajumbe 40; kati yao 20 ni kutoka Sekta ya Umma na 20 kutoka Sekta binafsi. Lengo kuu la Baraza la Biashara la Wilaya ni pamoja na kuwezesha mazingira mazuri ya kibiashara, kupitia na kujadili fursa na changamoto za kibiashara zilizopo katika Halmashauri pamoja na kung'amua fursa mpya kwa ajili ya uwekezaji ambazo zinaweza kuongeza mapato kwa wafanyabiashara na Halmashauri kwa jumla.

Kielelezo Na. 1: Picha ya kushoto inamuonesha mjumbe wa DBC akiwasilisha jambo katika kikao cha wadau. Picha ya kulia ni wajumbe wa DBC wakiwa wakijadiliana jambo muhimu kuhusu biashara.

SURA YA PILI

UFUMBUZI WA TATIZO

2.0 Utangulizi

Kabla ya kuanzishwa kwa Baraza la Biashara la Wilaya ya Kongwa mwaka 2014, Halmashauri ilikuwa inakabiliwa na changamoto nyingi za kibiashara. Aidha, kukosekana kwa jukwaa la majadiliano baina ya Halmashauri na wafanyabiashara kulisababisha migogoro mingi baina ya pande hizo mbili za Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Migogoro hii iliharibu uhusiano mzuri baina ya Halmashauri na wafanyabiashara. Kwa mfano, mivutano baina ya Halmashauri na wafanyabiashara ilisababisha kufunguliwa kesi katika Mahakama kwa kile kilichodaiwa kuwa Halmashauri imekuwa ikitoza ushuru mkubwa kwa mazao yanayouzwa katika soko la kimataifa la Kibaigwa. Hali hii ilichochewa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa Baraza la Biashara la Wilaya ambalo ni chombo cha majadiliano. Hali hii, sio tu ilifanya mazingira ya kibiashara kuwa magumu ndani ya Halmashauri, bali ilikatisha tamaa watu kuanzisha biashara mpya.

2.1.1 Malengo ya Mradi

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ilibaini kuwa pana uhusiano mbaya baina yake na Wafanyabiashara. Hali ilikuwa mbaya kiasi cha kufunguliwa kesi katika Mahakama ikipinga tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara. Pia, mapato ya Halmashauri yalishuka kutokana na wafanyabiashara wengi kugoma kulipa kodi na ushuru wa Halmashauri.

Baada ya kuanzishwa mradi wa LIC katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Uongozi wa Wilaya chini ya Mkurugenzi wa Wilaya, **Bi. Lilian Matinga** na Mkuu wa Wilaya, **Bw. Deogratius J. Ndejembi** uliweka malengo ya kuimarisha mazingira ya kibiashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa aliamua kulivunja Baraza la Biashara la Wilaya na kuliunda upya ili kuliongezea ufanisi. Shughuli ya uundaji Baraza jipya iliwashirikisha wadau kutoka LIC na wadau wengine wa biashara kutoka katika Halmashauri.

Aidha, ili kuongeza ufanisi wa Baraza, LIC imekuwa ikitoa kiasi cha Tsh 3,000,000 kufanikisha vikao vya kila mwezi vya baraza. Kwa kawaida, vikao hivi hufanyika kila baada ya robo ya mwaka. Kuanzia mwaka 2014 hadi 2018, Baraza limefanikiwa kukutana mara 28 kujadili mambo mbalimbali yanayohusiana na biashara ndani ya Halmashauri.

SURA YA TATU

MAFANIKIO, CHANGAMOTO, VIKWAZO, UIMARA NA MAFUNZO KUTOKA KATIKA MRADI

3.0 Matokeo na Mafanikio ya Mradi

Baaada ya kuanzishwa upya kwa Baraza la Biashara la Wilaya, kumekuwa na mafanikio makubwa ndani ya Halmashauri kama ifauatvyo:

1) Kuimarika kwa mahusiano baina ya Halmashauri/serikali na sekta binafsi (wafanyabiashara). Hali hii imechagizwa na kuwepo kwa jukwaa maalumu la kujadili fursa na changamoto za kibiashara ndani ya Wilaya. Aidha, pande hizi mbili zimekuwa zikishirikiana kutafuta suluhisho la matatizo mbalimbali yanayoviza ustawi wa biashara katika eneo husika.
2) Kupitia jukwaa la Baraza la Biashara la Wilaya kumesaidia kuongezeka kwa uwazi na ushirikishwaji wa wananchi katika mambo muhimu ya kibiashara ndani ya Halmashauri. Kwa mfano, Sekta binafsi imekuwa ikishiriki katika zoezi la uandaaji bajeti kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018.
3) Baraza la Biashara la Wilaya kwa kushirikiana na kikosi kazi cha Wilaya wamefanikiwa kufanya utafiti kuhusu tozo za biashara za mazao. Matokeo ya utafiti huu uliwasilishwa katika vikao vya Baraza la Halmashauri ambapo kulikuwa na mapendekezo ya kupunguza tozo mbalimbali. Kwa mfano, ilipendekezwa gunia la mahindi la kg. 100 litozwe Tsh. 1,500/= badala ya Tsh. 2,000/=, gunia la karanga la kg. 100 litozwe Tsh. 2,000/= badala ya Tsh. 3,000/= na gunia la mashudu ya alizeti litozwe Tsh. 500 badala ya Tsh. 1,000/=.
4) Kushiriki katika kubuni na uandishi wa miradi mbalimbali yenye lengo la kuimarisha mazingira ya kibiashara ndani ya Halmashauri.
5) Kuanzisha kanzi data ya kielektroniki. Mnano tarehe 2 Machi 2016 mfumo huu ulianza rasmi na umekuwa ukitumika kukusanyia mapato ya Halmashauri na kuweka kumbukumbu nyingine muhimu zinazohusiana na biashara.

6) Kuanzisha majukwaa maalumu ya kisheria kwa lengo la kutekeleza majukumu mbalimbali ya Baraza.
7) Kuajiriwa kwa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Biashara la Wilaya. Kwa kuanzia mtendaji huyu amepewa mkataba wa miaka miwili.
8) Kufanya tafiti kwa lengo la kubainisha changamoto mbalimbali zilizopo katika biashara ya mifugo ndani ya Halmashauri. Tafiti hizi zilisaidia sana kuinua mapato ya Halmashauri. Kwa mfano, kupitia mnada wa Dosidosi makusanyo yaliongezeka katika miezi mitatu kutoka Tsh. 486,000/= hadi kufikia Tsh. 990,000/=.
9) Uanzishwaji wa maeneo maalumu ya viwanda/maeneo ya kiuchumi katika maeneo ya Mbande na Kibaigwa.
    a) Eneo la uwekezaji la Kibaigwa lenye viwanja 40 (08/KBG/25/012018) na eneo la viwanda la Kibaigwa lenye viwanja 68 (08/KBG/26/012018);
    b) Eneo la viwanda la Ndurugumi lenye viwanja 74 (08/KBG/26/012018);
    c) Eneo la Mbande Kisimani lenye viwanja 78 (08/MBD/12/012018);
10) Kuongeza uwakilishi mpana wa wadau wa biashara katika Baraza la Biashara la Wilaya. Wadau hao ni pamoja na wakulima, waendeshaji bodaboda, wanawake, vijana, wasafirishaji, wamiliki wa vituo vya mafuta, wafanyabiashara wakubwa, wauzaji nyama, wakulima wa mbogamboga. Aidha, wadau hawa walitoka katika maeneo mbalimbali ndani ya Halmashauri.

3.1. Changamoto zinazolikabili Baraza la Biashara la Wilaya

1) Baraza la Biashara la Wilaya halifahamiki kwa wadau wengi waliopo vijijini. Hivyo, changamoto za watu wanaoishi vijijini hazijaweza kutatuliwa kupitia kazi za Baraza.
2) Hakuna uhakika kuwa Baraza litaendelea na shughuli zake baada ya kuisha kwa muda wa ufadhili wa LIC. Hii ni kutoka na ukweli kuwa hakuna uhakika kuwa pande mbili zinazounda Baraza hili litakuwa tayari kuendeleza shughuli za baraza.

3) Kukosekana kwa jukwaa maalumu la wafanyabiashara kutoka Sekta binafsi kujadili mambo yao kabla ya kuyawasilisha katika Baraza la Biashara la Wilaya kama inavyofanyika kupitia jukwaa la TPSF. Kwa hali hii, ni muhimu sana kuwepo na jukwaa/jumuiya itakayowakusanya wadau wa Sekta binafsi katika ngazi ya Halmashauri.

3.2. Vikwazo vya Ukuaji wa Biashara na Namna ya Kuvikabili

1) Ubovu wa miundombinu, ubovu wa barabara ya uhakika baina ya Kongwa na Mbande kunawanyima fursa wafanyabiashara kulifikia soko la kimataifa la Kibaigwa.
2) Kukosekana kwa taasisi za kielimu ndani ya Halmashauri kumesababisha kudorora kwa hali ya biashara. Halmashauri inafanya juhudi ya kuanzisha Chuo cha Ufundi (VETA) ili kuchochea mwingiliano baina ya wazawa na wageni na hivyo kuongeza fursa za kibiashara.
3) Uduni wa elimu ya biashara miongoni mwa wafanyabiashara. Tafiti zinaonyesha kuwa 70% ya wafanyabiashara hawana elimu kuhusu biashara wanazofanya (namna ya kutengeneza faida na kukabiliana na hasara, kutafuta masoko na namna ya kupanga bei).
4) Ukosefu wa mitaji, hali hii imesababisha kuwa na ugumu wa kuanzisha baishara mpya. Aidha, riba zimekuwa juu hali inayowamnyima fursa wananchi kukopa.
5) Ukosefu wa umeme wa uhakika;
6) Ugumu wa kupata maeneo ya uwekezaji, hii ni kutokana na ukweli kuwa maeneo mengi bado hayajapimwa.

3.3. Mipango ya Uimarishaji wa Mradi

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa iliamua kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Barazala la Biashara la Wilaya. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilitenga kiasi cha Tsh 3,075,000/= kutoka katika mapato yake ya ndani. Fedha hizi zililenga kufanikisha vikao muhimu vya Baraza.

3.4. Mafunzo Kutoka katika Mradi

1) Imebainika kuwa ni muhimu sana kuwa na viongozi wanaounga mkono ushirikiano baina ya Serikali na Sekta binafsi (PPDs). Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mradi umefanikiwa sana kutokana na ukweli kuwa kumekuwa na uungwaji mkono mkubwa wa mradi kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri.
2) Kuwepo kwa Baraza la Biashara la Wilaya katika Halmashauri hii ni kielelezo na somo zuri la kujifunza kwa Halmashauri zingine.
3) Baraza la Biashara la Wilaya limeleta mahusiano mazuri na kuondoa migogoro baina ya Halmashauri na wadau wa Sekta binafsi.
4) Baraza la Biashara la Wilaya limewezesha kupunguza tozo mbalimbali za mazao zilizokuwa kero kubwa kwa Wafanyabiashara.
5) Ni dhahiri kuwa Baraza la Biashara la Wilaya ndicho chombo pekee kinachowezesha wadau wa Sekta binafsi na Halmashauri kukaa pamoja na kujadili changamoto mbalimbali za kibiashara na namna ya kuzitatua.

SURA YA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.0 Hitimisho

Sehemu hii inajadili changamoto mbalimbali zinazolikabili Baraza la Biashara la Wilaya ya Kongwa sambamba na ufumbuzi wa changamoto hizo. Pia, sehemu hii inajadili namna Serikali na Sekta binafsi wanavyoweza kufanya kazi kwa ushirikianao kupitia jukwaa la Baraza la Biashara la Wilaya. Hii ni kusema kuwa, kitendo cha kuwa na Baraza la Biashara la Wilaya lililo imara kumeondoa changamoto nyingi zilizohusiana na biashara katika ngazi ya Halmashauri. Ni wazi kuwa, uimara wa Baraza la Biashara la Wilaya ni ufumbuzi wa matatizo mengi yanayohusiana na biashara katika ngazi ya Halmashauri.

4.1 Mapendekezo

Ili kuongeza ushirikiano baina ya Serikali na Sekta binafsi, andiko hili linatoa mapendekezo yanayolenga kuongeza ufanisi wa Baraza la Biashara la Wilaya kama ifuatavyo:

1) LIC iendelee kutoa misaada ya kifedha kwa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya nchini kote;
2) Kila Halmashauri ihakikishe kuwa inatenga bajeti maalumu kwa ajili ya uendeshaji wa Mabaraza ya Biashara ya Wilaya;
3) Kuwaelimisha wananchi wote kuhusu kuwepo na majukumu ya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya ili waweze kuyatumia kutatua changamoto mbalimbali za kibiashara;
4) Kuanzisha chombo maalumu kitakachowaunganisha wafanyabiashara wa Sekta binafsi. Aidha, chombo hiki kitaweza kutumika kuandaa ajenda za pamoja na kuziwasilisha katika vikao rasmi vya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:
Katibu Mkuu Mtendaji wa ALAT
S. L. P. 2049
Simu: +255 784 514 245
Dodoma, Tanzania
Barua pepe: info@alat.or.tz
Tovuti: www.alat.or.tz